

Juzi mwalimu wetu wa Somo la Kiswahili, Bwana Kituyi alitufunza kuhusu udogo wa nomino. Siku hiyo alikuja na vifaa halisi kama vile kigoma na kijijiti alivyoviweka kwenye kona. Alikuwa na kijitabu kidogo alichokitumia ambacho kilikuwa na kijikaratasi chenye vijisherufi vilivyosomeka kwa miwani tu. Ubaoni alichora picha ya kigombe kilichokonda na kukondeana. Aliandika nomino kadhaa ubaoni kama vile kijitu, kiatu, kibuzi, shamba, kijijino na kitambaa kisha akatuambia tutambue nomino za udogo kati ya nomino hizo.